# مُعَاوِيَةُ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ

الصَّحَابِيُّ الجَلِيْلُ وَالخَلِيْفَةُ الأَمِيْنُ وَأَمِيْرُ المُؤْمِنِيْنَ وَمُوَحِّدُ المُسْلِيْنَ عَامَ الْجَمَاعَةِ وَكَاتِبُ الوَحْيِ وَصِهْرُ سَيِّدِ المُرْسَلِيْنَ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ

# MU'AWIYA -ALLAAH AMRIDHIE-

## SWAHABA MTUKUFU, KHALIFA MUAMINIFU, AMIRUL MU'UMININ (KIONGOZI WA WAUMINI), ALIYEWAUNGANISHA WAISLAMU MWAKA WA UMOJA, MWANDISHI WA WAHYI NA SHEMEJI WA BWANA WA MITUME -SWALA NA SALAMU ZIMSHUKIE-


Mwandishi

Kamati ya wasomi wa Dar Al-Muntaqa

Tarjama

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

# YALIYOMO

1- Utangulizi ...3
2- Jina lake, Kun-ya yake na Kuzaliwa kwake -Allaah amridhie-...4
3- Kusilimu kwake...4
4- Wasifu wake kitabia na kimaumbile...5
5- Uandishi wake wa Wahyi...5
6- Elimu yake na Riwaya alizopokea...6
7- Mu'awiya ni miongoni mwa Maswahaba wa Mtume صلى الله عليه وسلم...7
8- Fadhila zake kiujumla...7
9- Fadhila zake makhsusi -Allaah amridhie- ...9
10-Nasaha za Mu'awiya -Allaah amridhie- kwa Raia wake...10
11-Barua zake -Allaah amridhie- na kufundisha kwake elimu ya kisheria...11
12-Kuhimiza kwake kufuata Sunnah na kutoikhalifu...11
13-Upole wake na Utukufu wake...12
14-Mu'awiya anamnyoa nywele Mtume -Swala na Salamu zimshukie-...13
15-Sifa za Maulamaa wa Salaf kwa Mu'awiya -Allaah amridhie- ...13
16-Ukhalifa wake -Allaah amridhie- ...15
17-Kifo chake -Allaah amridhie- ...15
18-Shia Ithnaasharia na uwongo wao dhidi ya Mu'awiya -Allaah amridhie-...16
19-Hitimisho...17

# Utangulizi

Sifa njema zote anastahiki Mola Mlezi wa viumbe wote. Swala na Salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad Mbora wa Mitume na Manabii, pia ziwashukie Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

## Ama baada ya hayo:

Bado swahaba Mu'awiya -Allaah amridhie- anakabiliwa na mashambulizi makali yaliyopangwa ili kuvunja heshima yake, na kupotosha historia yake iliyo nzuri, lakini pia kumtia dosari katika Dini yake na uadilifu wake, malengo makuu ya kampeni hii ni kufikia kuwashambulia Maswahaba wengine wakubwa, ambao ndio waliobeba Dini hii na kuisambaza, na wao ndio viongozi wa umma huu.

Maswahaba ndio watu wa mwanzo kuteremkiwa na Wahyi, kisha wakanukuu mafunzo hayo ya Uislamu kutoka kwenye kinywa cha Mtume wa umma huu -Swala na Salamu zimshukie- moja kwa moja pasi na kupitia kwa mtu wa kati, wakawa ni wenye kuihifadhi Dini hii katika **Mafunzo yake, Hukumu mbalimbali na Maana yake,** kwa sababu hiyo wamekuwa wao ndio daraja ambalo analikusudia adui mkubwa wa Uislamu **-Shia Ja'fariyya au Shia Ithnaasharia-** kulivunja ili kutimiza malengo yao ya kuubomoa Uislamu! Na haikuwa dhamira ya kumtusi Mu'awiyah -Allaah amridhie- isipokuwa ni kutaka kulivunja daraja hili Madhubuti.

Kwa ajili hiyo tumeandika risala hii fupi kwa lengo la kutaja wazi cheo cha Mu'awiyah -Allaah amridhie-, Fadhila zake, Elimu na Uadilifu wake, na kwamba yeye Mu'awiyah ni kama alivyosema Abu Ttauba Ar Rabii' Bin Nafii' Al-Halabiy: **"Mu'awiyah ni pazia kwa Maswahaba wa Mtume Muhammad -Swala na Salamu zimshukie-, basi mtu yeyote atakaefunua pazia (hilo) atapata ujasiri wa kile ambacho kipo nyuma yake[(1)]"[(2)].**

---

[1]- Maana yake: anaeweza kumtukana Mu'awiya basi ataweza kuwatukana Maswahaba wengine.
[2]- Tazama Kitabu: **[Al-Bidaayat Wan-Nihaya] (Jz. 8, Uk. 139)**.

## JINA LAKE, KUN-YA YAKE NA KUZALIWA KWAKE - رَضِيَ اللهُ عَنْهُ -

Nasaba ya Mu'wiyah inakutana na Nasaba ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kwa mzee Abdi Manaf[3].

**Jina lake ni:** Mu'awiyah Bin Abi Sufyan, (Abu Sufyan anaitwa) Swakhri Bin Ha'rbi Bin Umayyah Bin Abdi Shamsi Bin Abdi Manaf.

**Kun-ya yake ni:** Abu Abdil Rahman.

Naye ni mtu wa Makka, anatokana na kabila la Quraish katika ukoo wa Umyya (Al-Umawiy. Aliwahi kuwa kiongozi wa Waislamu wote (Amirul Muuminin), pia alikuwa Mwandishi wa Wahyi na ni Mfalme wa Uislamu,

**Mama yake ni:** Hindu Bint 'Utba Ibn Rabi'a Ibn Abdis Shams, lbn Abdi Manaf Bin Quswayyi.

Alizaliwa miaka mitano kabla ya Hijra (kabla Mtume -Swala na Salamu zimshukie- hajahama kutoka Makka kwenda Madina), na inasemekana ni kabla ya miaka saba, lakini kauli ya kwanza ina nguvu zaidi.

## KUSILIMU KWAKE MUA'WIYAH - رَضِيَ اللهُ عَنْهُ -

Amesema Imam Ddhahabiy -Allaah amrehemu: **"Mua'wiyah alisimu kabla ya Baba yake wakati wa Umrat Al-qadhwaa[4], na alishindwa kukutana na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kwa sababu ya kumuogopa Baba yake, na haukudhihiri Uislamu wake isipokuwa siku ya Fat'hu (Mwaka uliokombolewa mji wa Makka)"[5].**

---

[3]- Tazama kitabu: **[Siyaru a'laami Nnubalaa] (Jz. 3, Uk. 119).**

[4]- Umrat Al Qadhwaa ni Umra ambayo aliifanya Mtume -Swala na Salamu zimshukie- mfungo pili (Dhul-Qa'da) katika mwaka wa saba, alikaa Makka siku tatu kisha akarudi Madina.

5- Tazama kitabu: **[Siyaru A'laami Nnubalaa] (Jz. 3, Uk. 120).**

## WASIFU ZAKE KITABIA NA KIMAUMBILE - رَضِيَ اللهُ عَنْهُ -

Amesema Imam Ddhahabiy -Allaah amrehemu-: **"Ametaja Ibn Abi Ddun-ya na wengine kwamba Mu'awiyah alikuwa ni mrefu, mweupe, mzuri wa umbo, akicheka unabinuka mdomo wake wa juu, na alikuwa anazipaka rangi (ndevu zake). Na amepokea Said Bin Abdil Aziz kutoka kwa Abu Abdi Rabbi (amesema): Nilimuona Mu'awiyah anazipaka ndevu zake mmanjano, kana kwamba ni dhahabu (jinsi zinavyong'ara)"**[6].

**Ama sifa zake kitabia:** Amesema Sheikhul Islaam Ibn Taymiyyah -Allaah amrehemu-: **"Omar alimteua Mu'awiyah kuwa Gavana katika nafasi ya ndugu yake Yazid Bin Abi Sufyan, na akaendelea katika wadhifa huo muda wote wa Ukhalifa wa Omar, na (akawa) Omar na raia wake wanamshukuru yeye (Mu'awiyah) na wanashukuru mwenendo wake kwao, na wakawa wanampenda na wanaukubali uongozi wake, kwa yale waliyoyaona katika upole na uadilifu wake, kiasi ambacho hakuna yeyote miongoni mwao aliyepeleka mashtaka dhidi yake, wala kulalamika kudhulumiwa"**[7].

## UANDISHI WAKE WA WAHYI - رَضِيَ اللهُ عَنْهُ -

Imekuja katika Sahihi Muslim hadithi namba (2501), miongoni mwa hadithi za Abdullahi Bin Abbas -Allaah amridhie Yeye na Baba yake- amesema: **[Waislamu walikuwa hawamtazami Abu Sufyani wala hawakai naye pamoja, akasema (Abu Sufyan) kumuomba Mtume -Swala na Salamu zimshukie-: Ewe Mtume wa Allaah, nikubalie mimi mambo matatu, (Mtume) akamjibu: "Sawa". Akasema: Nikuozeshe Ummu Habiba Bint Abi Sufyan, mwanamke mzuri zaidi wa waarabu, akasema: "Sawa". Akasema: na huyu mwanangu Mu'awiya utamfanya kuwa mwandishi wako, akasema: "Sawa". Na unichague mimi niwe kiongozi ili nipambane na makafiri kama nilivyokuwa napambana na Waislamu, akasema: "sawa"].**

---

[6]- Tazama kitabu: **[Siyar a'alaami Nnubalaa] (Jz. 3, Uk. 120).**

[7]- Tazama kitabu: **[Majmuu'l Fataawa] (Jz. 4, Uk. 458).**

## ELIMU YAKE NA RIWAYA ZAKE - رَضِيَ اللهُ عَنْهُ -

Mu'awiyah -Allaah amridhie- amesimulia hadithi nyingi kutoka kwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na kutoka kwa dada yake (Ummu Habiba) Ummul Mu'minina (Mama wa Waumini), pia amesimulia kutoka kwa Abubakar na Omar -Allaah awaridhie-.

Ama waliopokea kutoka kwake hadithi ni Ibn Abbas -Allaah amridhie-, Said Bin Musayyab, Abu Saleh As Sammaany, Abu Idrisa Al Khaulaany, Salim Bin Abdillah, Muhammad Bin Siirin, na wengine wengi. Vilevile wamesimulia kutoka kwake Maswahaba wengi akiwemo: Jarir Bin Abdillaah, Abu Said, Nu'man Bin Bashir na Ibn Zubeir -Allaah awaridhie-.

Mu'awiyah -Allaah amridhie- alikuwa ni miongoni mwa wanachuoni wa Kiswahaba, imenukuliwa kwake Elimu nyingi, Fatawa na Hukumu mbalimbali za Dini, kama alivyothibitisha hilo Ibn Abbas -Allaah amridhie- wakati alipoulizwa: **[Je, unasemaje kuhusu Amiril Mu'miniin Mu'awiyah, kwani yeye haswali witri isipokuwa rakaa moja tu! Akasema: "Amepatia, yeye ni Faqih (mtambuzi wa Dini)"]**[8].

Na pia imekuja katika [Musnad As Shafi']**[9]** na [Tareikh Dimashki]**[10]**, kwamba Kuraib (mtumwa aliyeachwa huru na Ibn Abbas) alimsimulia (Ibn Abbas) kwamba yeye alimuona Mu'awiyah ameswali swala ya Ishaa kisha akaswali witri rakaa moja bila kuzidisha chochote,.. akasema Ibn Abbas: **"Ewe kijana wangu amepatia, hakuna yeyote katika sisi mjuzi zaidi ya Mu'awiyah, hiyo (witri) ni rakaa moja au tano, saba, na zaidi ya hapo kiasi anachotaka".**

---

[8]- Tazama kitabu: **[Sahihi al Bukhari] (3765).**
[9]- Tazama kitabu: **[Musnad As Shafii] (Jz. 1, Uk. 10).**
[10]- Hadithi (63843)

## MU'AWIYAH - رَضِيَ اللهُ عَنْهُ - NI KATIKA SWAHABA WA MTUME -صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ-

Imetangulia ya kwamba Mu'awiyah -Allaah amridhie- alisilimu kabla ya Fat'hu Makka na pia alikuwa miongoni mwa waandishi wa Wahyi, kwa hiyo yeye ni miongoni mwa Maswahaba wenye fadhila na daraja kubwa kama walivyo Maswahaba wengine, na ataingia katika jumla ya wale ambao Allaah amewasifu katika Aya nyingi ndani ya Qur'an kwa kumuamini kwao Mtume wake -Swala na Salamu zimshukie-, kusuhubiana kwa wema na kumnusuru.

## FADHILA ZA MU'AWIYAH KIUJUMLA - رَضِيَ اللهُ عَنْهُ -

Hapana shaka yoyote kwamba Mu'awiyah -Allaah amridhie- anaingia kiujumla katika Aya ambazo zimekuja kuwasifu Maswahaba -Allaah awaridhie-, miongoni mwa Aya hizo ni:

﴿ مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ ٱللَّهِ ۚ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلْكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيْنَهُمْ ۖ تَرَىٰهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضْوَٰنًا ۖ سِيمَاهُمْ فِى وُجُوهِهِم مِّنْ أَثَرِ ٱلسُّجُودِ ۚ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمْ فِى ٱلتَّوْرَىٰةِ ۚ وَمَثَلُهُمْ فِى ٱلْإِنجِيلِ كَزَرْعٍ أَخْرَجَ شَطْـَٔهُۥ فَـَٔازَرَهُۥ فَٱسْتَغْلَظَ فَٱسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوقِهِۦ يُعْجِبُ ٱلزُّرَّاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ ٱلْكُفَّارَ ۗ وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ مِنْهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًۢا ﴾

**"Muhammad ni Mtume wa Allaah. Na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri na wanahurumiana wao kwa wao. Utawaona wakirukuu na kusujudu wakitafuta fadhila za Allaah na radhi zake. Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu. Huu ndio wasifu wao katika Taurati. Na wasifu katika Injili ni kama mmea uliotoa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya ubuwa wake, ukawafurahisha wakulima, ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri. Allaah amewaahidi walio amini na wakatenda mema katika jinsi yao msamaha na ujira mkubwa)[(11)].**

[11]- Surat Al Fat-h/29.

Lau isingeteremka Aya kuhusu fadhila za Maswahaba isipokuwa Aya hii tu basi ingetosheleza.

Na Allaah amesema:

﴿وَٱلسَّٰبِقُونَ ٱلۡأَوَّلُونَ مِنَ ٱلۡمُهَٰجِرِينَ وَٱلۡأَنصَارِ وَٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُم بِإِحۡسَٰنٖ رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنۡهُمۡ وَرَضُواْ عَنۡهُ وَأَعَدَّ لَهُمۡ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي تَحۡتَهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدٗاۚ ذَٰلِكَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡعَظِيمُ﴾

**"Na wale walio tangulia, wa mwanzo, katika Muhajirina na Ansari, na waliowafuata kwa wema, Allaah ameridhika nao, na wao wameridhika naye, na amewaandalia Bustani ambazo inapita mito chini yake, hali ya kukaa humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa"[(12)].**

Pia anasema:

﴿وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَهَاجَرُواْ وَجَٰهَدُواْ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱلَّذِينَ ءَاوَواْ وَّنَصَرُوٓاْ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ حَقّٗاۚ لَّهُم مَّغۡفِرَةٞ وَرِزۡقٞ كَرِيمٞ﴾

**"Na wale walio amini wakahama na wakapigana Jihadi katika njia ya Allaah, na wale waliotoa mahala pa kukaa (kwa waliohamia mji wao) na wakanusuru, hao ndio waumini wakweli. Watapata msamaha wa Allaah na kuruzukiwa kwema"[(13)].**

Na amesema:

﴿لَا يَسۡتَوِي مِنكُم مَّنۡ أَنفَقَ مِن قَبۡلِ ٱلۡفَتۡحِ وَقَٰتَلَۚ أُوْلَٰٓئِكَ أَعۡظَمُ دَرَجَةٗ مِّنَ ٱلَّذِينَ أَنفَقُواْ مِنۢ بَعۡدُ وَقَٰتَلُواْۚ وَكُلّٗا وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلۡحُسۡنَىٰۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعۡمَلُونَ خَبِيرٞ﴾

**"Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa kabla ya ushindi (fat-hu ya Hudaibiya) na wakapigana vita. Hao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale ambao walitoa baadae na wakapigana. Na wote hao Allaah amewaahidi pepo"[(14)].**

---

[12]- Surat At Tawba/100.
[13]- Surat Al Anfaal/74.
[14]- Surat Al Hadid/10.

Na Aya nyingine nyingi zilizokuja kuwasifu Maswahaba.

Ama hadithi zilizokuja kuwasifu Maswahaba akiwemo Mu'wiyah -Allaah awaridhie- nyingi sana, miongoni mwa hizo:

Hadithi ya Abu Said Al Khudriy -Allaah amridhie- amesema, amesema Mtume -Swala na Salamu zimshukie-: **"Msiwatukane Maswahaba zangu, lau mmoja wenu alitoa dhababu mfano wa mlima Uhud (basi) hatofikia kibaba cha mmoja wao wala nusu yake[15]"[16].**

## FADHILA ALIZOPWEKEKA NAZO MU'AWIYAH - رَضِيَ اللهُ عَنْهُ -

Mu'awiyah -Allaah amridhie- ndiye mtu wa mwanzo kupigana Jihadi kwa njia ya bahari, na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amesema: **"Jeshi la mwanzo katika umma wangu litakalopigana jihad kwa njia ya bahari limesamehewa…"[17].**

Amesema Ibn Hajar -Allaah amrehemu-: **"Amesema Al Muhallab: Katika hadithi hii kuna fadhila za Mu'awiyah kwa sababu yeye ndiye mtu wa mwanzo kupigana kwa njia ya bahari"[18].**

Pia amesema Ibn Abdil Barri -Allaah amrehemu-: **"Kuna katika hadithi hii fadhila za Mu'awiyah, kwani wamejaaliwa kuwa watu mwanzo kupigana "kwa baharini" walikuwa chini ya uongozi wake"[19].**

Vita hivi vilipaganwa katika kisiwa cha Qubrus hivi sasa inaitwa (Syprus) chini ya Amiri jeshi Mu'wiyah -Allaah amridhie-.

---

[15]- Hii ni alama ya kuonesha ukubwa wa Imani ya Maswahaba -Allaah awaridhie-.
[16]- Tazama kitabu: **[Sahihi al Bukhari] (3673) na Muslim (2540).**
[17]- Tazama kitabu: **[Sahihi al Bukhari] (2924).**
[18]- Tazama kitabu: **[At Tamhid] (Jz. 1, Uk. 235).**

Amesema Mtume -Swala na Salamu zimshukie- akimkusudia mjuu wake Hassan Bin Ally -Allaah amridhie Yeye na Baba yake-: **"Hakika mtoto wangu huyu ni bwana, na Allaah atasuluhisha kupitia yeye baina ya makundi mawili makubwa ya Waislamu"**[20].

Hii ni dalili ya wazi kutoka kwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- akisifia kundi la Hassan -Allaah amridhie- na wale walio pamoja naye na kundi la Mu'wiyah -Allaah amridhie- na wale walio pamoja naye, kwamba ni makundi mawili makubwa ya Waislamu, na wala hakutafautisha baina yao, kwa maana makundi mawili hayo yanalingana sawa katika fadhila na utukufu.

Na katika hadithi nyingine Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alimuombea dua Mu'awiyah kwa kusema: **"Ewe Allaah, mfahamishe Mu'awiyah Qur'an na Hesabu, na mkinge na adhabu"**[21].

## NASAHA ZA MU'AWIYAH -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ- KWA RAIA WAKE

Alikuwa Mu'awiyah -Allaah amridhie- ni mtu anayependa kheri kwa Waislamu, imepokewa kutoka kwa Abu Uthman As Shaami -Allaah amrehemu-: **"Alikuwa Mu'awiyah anatutokezea hali ya kuwa sisi tupo katika madrasa (za kusomesha watoto Qur'an) na anasema kumwambia mwalimu: Ewe mwalimu, wafundishe watoto wa Muhajirina maadili mema"**[22].

Na alikuwa akisema kuwaambia raia wake: **"Tahadharini na fitna msiipupie, kwa sababu (fitna) inaharibu Maisha, inapunguza neema, na inapelekea kwenye kuadimika (kwa bidhaa)"**[23].

---

[20]- Tazama kitabu: **[Sahihi al Bukhari] (2557).**
[21]- Tazama: **[Sahihi Ibn Khuzaima] (1938), [Ibn Hibban] (2782), [Ahmad] (Jz. 4, Uk. 127) na [As Sahiha].**
[22]- Tazama kitabu: **[An Nafaqatu alal 'Iyaal] (Uk. 293) cha Ibn Abi Ddun-ya.**
[23]- Tazama kitabu: **[Siyar a'laami Nnubalaa] (Jz. 2, Uk. 148).**

## BARUA ZA MU'AWIYAH -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ- NA KUFUNDISHA KWAKE ELIMU YA KISHERIA

Imepokewa kutoka kwa Ibn Abi Shihab, amenisimulia Humeid amesema: Nimemsikia Mu'awiyah Ibn Abi Sufyan akihutubia akasema: **"Yule ambaye Allaah anamtakia kheri humpa Fiqhi (utambuzi) katika Dini"**[24].

Na imepokewa kutoka kwa Warraad Mwandishi wa Mughira amesema: **[Mu'awiyah aliandika barua kwenda kwa Mughira (kwamba): Niandikie mimi yale uliyoyasikia kutoka kwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-; akamuandikia: "Hakika Mtume wa Allaah -Swala na Salamu zimshukie- alikuwa akisema kila baada ya swala: Laa ilaaha illa Llaahu wahdahu laa shariikalahu, lahul Mulku, walahul hamdu, wahuwa 'alaa kulli shay-in Qadir. Allaahumma laa maani'a limaa a'twaita, walaa mu'twiya limaa mana'ta, walaa yanfa'u dhal-jaddi minkal jaddu". Na alimuandikia kwamba: "Na alikuwa anakataza porojo (mazungumzo yasiyo na faida), na wingi wa kuuliza maswali, na kuifuja mali. Na pia alikuwa anakataza kuwaasi wazazi wa kike (mama) na kuwazika Watoto wa kike ilihali wakiwa hai, na kuzuia haki za watu na kuchukua mali zao pasi na haki"]**[25].

## KUHIMIZA KWAKE KUFUATA SUNNAH NA KUTOIKHALIFU

Alikuwa Mu'awiyah -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ- anawahimiza watu kufuata hadithi za Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na anawakataza wao kutokwenda kinyume nazo, alikuwa anakija katika mji wa Madina na akapata habari ya jambo lililofanywa na wanachuoni wa mji huo ambalo linakhalifu Sunnah, anawaambia watu wa Madina: **"Wako wapi wanachuoni wenu, mimi nimemsikia Mtume -Swala na Salamu zimshukie- akisema hvi, (au) nimemuona akifanya hivi"**[26].

---

[24]- Tazama kitabu: **[Sahihi al Bukhari] (71) na Muslim (1037).**
[25]- Tazama kitabu: **[Sahihi al Bukhari] (7292).**
[26]- Tazama kitabu: **[Fat-hul Baary] (Jz. 6, Uk. 516).**

Na ametaja Imam Muslim -Allaah amrehemu- kutoka kwa 'Amru Bin 'Atwaa amesema: **[Naafi' Bin Jubeir alimtuma yeye kwenda kwa As Saaib kumuuliza jambo ambalo alimuona Mu'awiyah akilifanya katika swala yake, akasema (As Saaib): Ndio, niliswali pamoja naye swala ya Ijumaa katika sehemu inayoitwa Maqsuura, wakati alipomaliza nilisimama na kuswali (sunna) katika sehemu yangu hiyo hiyo (niliyoswali faradhi), akaniita na akaniambia: "Usirudie tena vile ulivyofanya, utakapomaliza kuswali swala ya Ijumaa usiunganishe na swala nyingine mpaka uzungumze au utoke (sehemu hiyo uliyoswali faradhi"]**[27].

Na alikuwa ni mwingi wa kuitukuza sunnah, kuwafundisha watu na kuitawanya, ndiyo maana aliwahi kumuandikia Mughira akimtaka amwambie kile alichomsikia Mtume -wala na Salamu zimshukie- miongoni mwa Adhkaar anazosoma baada ya kumaliza swala ya faradhi[28].

## UPOLE WAKE NA UTUKUFU WAKE -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ-

Mu'awiyah -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ- alifahamika kwa upole na uadilifu wakati alipokuwa Gavana wa Sham, na ilikuwa Siasa anayoitumia kwa raia wake ni Siasa bora, mpaka wakawa wanampenda naye anawapenda, amesema Abdullaahi Ibn Umar -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ- : **"Alikuwa Mu'wiyah ni mpole zaidi kwa watu, watu wakamuuliza: Ewe Abu Abdil Rahman: Je Abubakar? Akasema: Abubakar -رضِيَ اللهُ عَنْهُ- ni mbora kuliko Mu'awiyah, na Mu'awiyah ni mpole zaidi kwa watu"**[29].

---

[27]- Tazama kitabu: **[Sahihi Muslim] (883).**
[28]- Tazama kitabu: **[Bukhari] (6615).**
[29]- Tazama kitabu: **[As Sunnah Liabii Bakar Bin Khallaal] hadithi namba (680).**

## MU'AWIYAH -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ- ANAMNYOA NYWELE MTUME -صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ-

Imepokewa kutoka kwa Twaus -Allaah amrehemu- amesema: Amesema Ibn Abbas -Allaah amridhie- (siku moja) Mu'wiyaha aliniuliza: **"Hivi unajua kwamba mimi niliwahi kumnyoa (nywele) Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kwa kisu kipana tulipokuwa Marwa"**[30].

## MAULAMAA WA SALAF WAKIMSIFU MU'AWIYAH - رَضِيَ اللهُ عَنْهُ -

Hakika Mu'awiyah -Allaah amridhie- amepata sifa nyingi kutoka kwa Maulamaa mbalimbali wa Kisalafi (wema waliotangua), nao ni watu waaminifu zaidi na wenye nguvu zaidi kwa Imani, kwa hiyo ushahidi wao una nguvu zaidi katika kuthibitisha ukweli wake na utukufu wa daraja lake, kama ilivyo kwa Maswahaba wengine, na huu ndio ushahidi wao:

1) Aliulizwa Abdullah Bin Mubarak -Allaah amrehemu-, Ni yupi bora: Mu'awiyah Ibn Abi Sufyan au Umar Ibn Abdil Aziz? Akasema: **"Hakika vumbi ambalo limeingia puani mwa Mu'wiyah akiwa pamoja na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- ni bora zaidi kuliko Umar Ibn Abdil Aziz"**[31].
2) Imepokewa kutoka kwa Al-Jarraah Al-Mauswiliy -Allaah amrehemu- amesema: [Nilimsikia mtu mmoja akimuuliza Mu'afaa Bin Imran -Allaah amrehemu-: Ewe Abu Masoud, ni ipi nafasi ya Umar Bin Abdil Aziz kwa Mu'awiyah Bin Abi Sufyan? Nikamuona amechukia sana akasema: **"Haifai kupigiwa kiasi swahaba wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na mtu yeyote. Mu'awiyah -Allaah amridhie- ni Swahaba wake, Mwandishi wake (wa wahyi), Shemeji yake, na Muaminifu wake katika Wahyi"]**[32].

---

[30]- Tazama kitabu: **[Sahihi al Bukhari] (1370) na [Muslim] (1246),** na tamko hili ni la Imam Muslim.
[31]- Tazama kitabu: **[As Sharii'ah Lil-Aajurry] (Jz. 5, Uk. 2466).**
[32]- Tazama kitabu: **[As Shariia'h Lil-Aajurry] (Jz. 5, Uk. 2466).**

3) Imesimuliwa kutoka kwa Abu Usama -Allaah amrehemu- kwamba siku moja aliulizwa: Ni yupi bora Mu'awiyah au Umar Bin Abdil Aziz? Akasema: **"Hakuna mtu yeyote ambaye hupigiwa kiasi na Maswahaba wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-"**[33].
4) Na amesema Abdullah Bin Mubarak -Allaah amrehemu- **"Mu'awiyah kwetu sisi ni mtihani, tukimuona mtu yeyote anamtazama yeye kwa jicho la dharau tutamtuhumu yeye kuwa anawadharau hata Maswahaba wengine"**[34].
5) Aliulizwa Imam Ahmad -Allaah amrehemu-: [Unasemaje (Allaah akurehemu) kuhusu mtu ambaye anasema kwamba: Mimi sikubali kwamba Mu'awiyah alikuwa ni Mwandishi wa Wahyi, na wala siamini kwamba yeye ni mjomba wa waumini, kwani yeye alichukua Ukhalifa kwa mabavu. Akasema Abu Abdillaah (imam Ahmad): **"Hii ni kauli mbaya, watu hao (wanastahiki) kutengwa wala haifai kukaa pamoja nao, na tutalibainisha jambo lao kwa watu"]**[35].
6) Imepokewa kutoka kwa Abu Twalib, kwamba yeye alimuuliza Abu Abdillaah (Imam Ahmad): [Je Mu'awiyah ni mjomba wa Waislamu? Je Ibn Umar ni mjomba wa Waislamu? Akasema: **Ndio, Mu'awiyah ni ndugu na Ummu Habiba Binti wa Abu Sufyan Mke wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, na Ibn Umar ni ndugu na Hafsa (binti Umar) Mke wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- Allaah awarehemu.** Nikasema: Je Mu'wiyah ni mjomba wa Waislamu? Akajibu: **Ndio"]**[36].
7) Imepokewa kutoka kwa Ibrahim Al Harbiy amesema: [Nilimsikia Ahmad Bin Hambal wakati mtu mmoja alipomuuliza: Ewe Abu Abdillaah, Mimi nina mjomba wangu, inasemekana kwamba yeye anamtukana Mu'wiyah, na huenda nikala pamoja naye, Imam Ahmad akajibu kwa haraka hali ya kusema: **"Usile pamoja naye".** Tazama: **[As Sunnah Lil Khallaal] (693).**

---

[33]- Tazama: **[As Shariia'h Lil-Aajurry] (Jz. 5, Uk. 2466).**
[34]- Tazama kitabu: **[Al- Bidayat wan-Nihayat] (Jz. 8, Uk. 148).**
[35]- Tazama kitabu: **[As Sunnah Lil Khallaal] (643).**
[36]- Tazama kitabu: **[As Sunnah Lil Khallaal] (657).**

## UKHALIFA WAKE -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ-

Mu'awiyah alitawala muda wa takriban miaka ishirini, mpaka ukafika mwaka ambao alifanya sulhu yeye na Hassan mjukuu wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- sulhu ambayo Mtume -Swala na Salamu zimshukie- aliwahi kuitolea bishara, ikawa ni kheri kwa Umma wa Kiislamu, kwani ziliungana safu zao, na kuwa moja neno lao, na Waislamu wakarudi tena kwenye kupigana Jihadi na maadui zao, na kuifungua miji (ya makafiri) na kuieneza elimu na da'wa, ikathibiti kauli ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie- pale aliposema kuhusu Hassan -Allaah amridhie-: **"Hakika kijana wangu huyu ni Bwana, na huenda Allaah akasuluhisha kupitia yeye baina ya makundi mawili makubwa miongoni mwa Waislamu"**. **[Sahihi al Bukhari] (2557).**

Na kwa sababu hii katika Ukhalifa wa Mu'awiyah ulipatikana ufunguzi wa miji mingi na kukombolewa kutoka mikononi mwa makafiri, hasa upande Roma, Maghrib, Kaskazini mwa Africa, na upande wa Mashariki, Sijistan, Khurasaan, na miji iliyo nyuma ya mto Sihoni na Gihoni, kama vile: (Samarkand, Uzbekistan, Kazakhstan n.k.).

Amesema Imam Ddhahabi -Allaah amrehemu- wakati akifanya ufupisho wa khilafa ya Mu'awiyah -Allaah amridhie-: **"Alikuwa anapendwa na raia wake, amekaa Gavana huko Sham miaka ishirini, na akakaa kwenye Ukhalifa miaka ishirini pia, na hakuna mtu yeyote aliyemkejeli katika uongozi wake, bali mataifa mengi yalijiweka karibu naye, na akawatawala Waarabu na Waajemi, na utawala wake ulikuwa Makka na Madina, Misr, Sham, Iraq, Khurasan, Persia (Fursi), Yemen, n,k".** Tazama kitabu: **[Siyar A'laami Nnubalaa] (Jz. 3, Uk 133).**

## KIFO CHAKE -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ-

Amefariki huko Damascas (Syria) siku ya Al khamis ya mwezi wa rajab mwaka 60$^{H}$, baada ya kuishi miaka mingi akiwa katika Imani, Jihad, na kuifungua miji mbalimbali na kueneza Uislamu. **[Al Bidaaya] (Jz. 8, Uk. 123).**

## SHIA ITHNAASHARIA NA UWONGO WAO DHIDI YA MU'AWIYA -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ-

Si jambo lenye kufichikana kwa Waislamu kuhusu msimamo wa Shia Ithnaasharia dhidi ya Maswahaba wa Bwana Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kiujumla, hasa swahaba Mu'awiya -Allaah amridhie-.

Hakika Mashia wamezua hadithi nyingi za uwongo dhidi ya swahaba Mu'awiya -Allaah amridhie- na kuzieneza, pia wametumia fursa katika matukio yaliyojiri baina ya Maswahaba na hasa tukio la Mu'awiya na Ally -Allaah awaridhie-, ndiyo maana utapata riwaya zilizokuja kumtaja vibaya Mu'awiya na kutia dosari historia yake wapokezi wake ni Mashia Raafidhwa, watu waongo wenye kutunga hadithi, lakini maulamaa wa Kiislamu tangu hapo mwanzo hawakulala, bali walisimama kubainisha uharibifu wao huo na kuziweka wazi riwaya zao hizo mbovu ili asije muislamu kunasa kwenye mtego wao huo, kwa sababu hii, ewe ndugu muislamu, tahadhari na kusoma vitabu vya Tareikh (historia) bila kurudi kwa Maulamaa wabobezi wa jambo hilo, kadhalika tahadhari na kuziamini riwaya za wapokezi waongo kama vile Lut Bin Yahya Abu Mikhnaf, Nasru Bin Muzaahim Al Kalbiy na mfano wao.

Na amesema kweli Imam Malik Bin Anas - Allaah amridhie- wakati akiwaelezea Shia: **"Hawa ni watu ambao wamekusudia kumkejeli Mtume -Swala na Salamu zimshukie- lakini hawakuweza, wakawakejeli Maswahaba zake ili pasemwe: (kumbe Muhammad) ni mtu muovu, na lau angelikuwa ni mtu mwema basi Maswahaba zake wangelikuwa wema pia"**[37].

[37]- Tazama kitabu: **[As Swaarimul masluul] (Uk. 580).**

## HITIMISHO

Hii ndiyo historia fupi yenye kuvutia kuhusu fadhila za Swahaba Mu'awiya -Allaah amridhie- Mjomba wa waumini, kwa hakika ni historia ambayo inampasa kila muislamu kuijua, ili amfahamu swahaba huyu mtukufu na kufahamu nafasi yake katika Uislamu, kadhalika wapate kuijua njia ya wakosefu maadui wa Uislamu ambao wamejenga misingi ya Dini yao katika kuwatusi Maswahaba wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- hasa huyu Mu'awiya -Allaah amridhie-.

Na kauli ya kukata shauri kuhusu fadhila za Mu'awiya ni maneno ya Abdullaah Bin Mubarak -Allaah amrehemu-: **[Mu'awiya ni mtihani kwetu, yeyote tutakaempata anamtazama (Mu'awiya) kwa dharau, tutamtuhumu (kwamba anawadharau) hata kwa Maswahaba wengine]**[38].

**Na Swala na Salamu zimshukie mja wake na Mtume wake Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba zake wote.**

**Abu Halima Arafat Bin Mahmoud**

**Leo 8/shaban/1445H – 18/2/2024M**

**Tanzania.**

[38]- Tazama kitabu: **[Al Bidaya wan Nihaya] (Jz. 8, Uk. 148).**